

## Arusha waanza mchakato uvalishaji hereni mifugo

Na Veronica Mheta, Arusha

**H**ALMASHAURI ya Arusha itanza utambuzi wa mifugo 25,000 kwa awamu ya kwanza, ikiwa ni utekelejazi wa agizo la serikali la kualishisha mifugo hereni za kielectroniki.

Lengo ni kutambua idadi ya mifugo, mmiliki wake pamoja na eneo inapotokea.

Akizungumza wakati wa kupoea hereni hizo kutoka kampuni ya S&J, Daktari wa Mifugo wa Halmashauri ya Arusha, Yohana Kiwone alisema wanepokea hereni hizo kutoka kampuni hiyo kwa ajili ya uvalishaji mifugo.

Alisema katika Halmashauri ya Arusha utambuzi utafanyika kwa awamu nne, ambapo jumla ya mifugo 200,019 itavashwa hereni hizo za kielectroniki, wakawamo ng'ombe 81,550, punda 3,535, mbuzi 60,671 na kondoo 54,245, huku awamu ya kwanza ikitegemea kuvikwa hereni mifugo 25,000.

Dk Kiwone aliwataka wafugaji wote wa Halmashauri ya Arusha kuwa tarayi kutekeleza agizo hilo la serikali na kueleza kuwa mifugo ambayo itavikwa hereni hizo ni ng'ombe, mbuzi, kondoo na punda.

"Kila mifugaji atagharamia hereni kwa mifugo yake, bei ya ng'ombe na punda ni Sh 1,750 na bei ya mbuzi na kondoo itakuwa Sh 1,000 kwa kila mifugo, hivyo wafugaji wote wanapaswa kujitokeza," alisema.

Alizitaja faida za kuvalisha mifugo hereni za kielectroniki ni kutambua mifugo kulingana na umiliki na eneo inapotokea, kidhibiti wizi wa mifugo na magonjwa, kui-marisha soko la ndani na rje la bidhaa za mifugo pamoja na kutatta migogoro baina ya wakulima na wafugaji inayojitokeza mara kwa mara nchini.

Utambuzi wa mifugo kwa njia ya kielectroniki unaafanyika kwa mujibu wa sheria ya utambuzi, usajili na ufuatilaji ya mwaka 2012, inayolekeza kutumia hereni za kielectroniki na taarifa za mifugo na mifugaji zitachukuliwa kwenye nakala ngumu na nakala za kielectroniki na kuingizwa kwenye kanzi data ya taifa.

# Wakulima wata subira bei ya ml

Na Mwandishi Wetu, Sumbawanga

**W**AKULIMA wametakiwa kuwa na subira wakati serikali ikichukua hatua za muda mfupi na mrefu za kupunguza bei ya mbolea ambayo kwa sasa ipo juu sokoni.

Kauli hiyo ilitolewa na Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunda wakati akizungumza na wananchi wa Rukwa katika eneo la kiwanda cha kusindika mahindi cha Fantashiru, wakati wa ziara ya Rais mstaafu, Jakaya Kikwete ambaye ni mjumbe wa Bodi ya Shirika la Mapinduzi ya Kijani Barani Afrika (Agra).

Alisema kupanda kwa bei ya mbolea kutoka Sh 60,000 na 70,000 hadi Sh 110,000 au Sh 120,000 kumetokana na kupungua kwa mbolea sokoni kulisababishwa na janga la Covid-19 duniani.

Alisema ugonjwa huo umesababisha usafirishaji na uzalishaji wa mbolea kutoka nije kuwa mgumu na hivyo bei kupanda.

Mmoja wa waku-

lima wakizungumza na Dk Kikwete kuhusu mafanikio yao kutokana na uwapo wa miradi mbalimbali ya Agra ambaye ni mmliki wa kampuni ya Fantashiru, Anwar Said alisema wakati bei ya mahindi ipo chini, ununuzi wa pembejeo una gharama kubwa.

Mavunde alisema serikali imejipanga kuondoa tatzio hilo kwa kuweka mazingira wezeshi ya sekta binafsi kwa kushirikiana na serikali ili kuwapo na mbolea ya kutosha.

Alisema ifikapo Ju-lai mwaka huu kiwanda kikubwa kitakachozalisha tani 600,000 za mbolea kwa mwaka kitaanza kazii na kupunguza uagizaji wa pembejeo hiyo kutoka nje.

Aliwataka wananchi kutambua kwamba serikali imeweka mazingira wezeshi ya wadau kuweza kushirikili kutatua changamoto hiyo ikiwamo uwapo wa mwekezaji huyo wa

Burundi ambaye ujenzi wa kiwanda chake umefika asilimia 55.

Alisema kabla ya kiwanda hicho hakijaanza kufanyakazi,



## NMB Masta Bata yap moto, zawadi zafikia i

Na Mwandishi Wetu

**W**ATEJA 100 wa Benki ya NMB wamejinyakulia Sh milioni 10 katika droo ya wiki ya saba ya msimu wa tatu wa kampeni ya 'NMB MastaBata-Kivyo Vyako' inayoendeshwa na Benki hiyo.

Droo hiyo ilifanyika jana Dar es Salaam na kufanya washindi wa droo hizo kufikia 725, waliojinyakulia Sh milioni 95 katika wiki saba kati ya 10 za kampeni hiyo.

MastaBata ni kampeni inayoendeshwa na NMB kwa lengo la kuhamasisha matumizi ya kadi, kufanya malipo na manunu kwa MasterCard, Masterpass QR, Vituo ya Mauzo (PoS), ambapo imetenga zaidi ya Sh milioni 200 kama motisha kwashindi wa droo za wiki, mwezi na 'Grand Finale.'

Katika kampeni hiyo, washindi 100 wa wiki hujishindia Sh 100,000 kila mmoja, wakati washindi 25 wa droo za mwezi kila mmoja hujishindia shilingi milioni moja, huku wateja 30 wakitarajiwai kuzoa shilingi milioni 3 kila mmoja katika fainali ya kuhitimisha NMB MastaBata mwishoni mwa mwezi Machi.

Ofisa wa Kitengo cha Kadi wa Benki ya NMB, Lightness Zablon, alisema kumekuwa na mutikio mkubwa miuongoni mwa wateja wa benki hiyo kutumia kadi zao katika kupata huduma hasa katika vituo vya mafuta, maduka makubwa (supermarket), PoS, migahani na mtandaoni.

Zablon alisema kuwa wanajivunia ongezeko la wateja wanaoenda na mabadiliko ya teknolojia yanayochagiza matumizi yasiyohusisha pesa taslimu, huku akisisitiza